ISSN 2820-2686 | Toleo Na. 7 | Aprili - Juni 2023

# JARIDA LA WAKILI MKUU








# BODI YA UHARIRI

## Mwenyekiti

**Sarah Duncan Mwaipopo**
Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

## Mhariri Mkuu

**Prisca Jackson Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

## Waandishi wa Jarida

**Prisca Jackson Ulomi**
Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**Dennis Julius Buyekwa**
Afisa Habari

**Stanley Kalokola**
Wakili wa Serikali

**Neisha Shao**
Wakili wa Serikali

## Msanifu wa Jarida

**Nyamhoni Robert Chacha**
Afisa TEHAMA

## Wajumbe

**George Nathaniel Mandepo**
Mkurugenzi wa usuluhishi

**Hangi Matekeleza Chang'a**
Mkurugenzi Msaidizi Katiba, haki za binadamu na Uchaguzi

**Kiuye Mbwana Shemakame**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti

**CPA Devota Mathew Ngulugulu**
Mhasibu Mkuu

**Mercy Rowland Kyamba**
Mkurugenzi Msaidizi - Udhibiti Ubora

**Zuhura Mohamed Kussaga**
Mchumi

# TAHARIRI

Tarehe 05 Juni, 2023; Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliadhimisha miaka mitano tangu kuanzishwa kwake ambapo Mgeni Rasmi wa Maadhimisho hayo alikuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungamo wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) ambapo maadhimisho hayo yalikuwa na kauli mbiu isemayo, "Miaka Mitano ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali: Tulipotoka, Tulipo na Tunapoelekea."

Kufanyika kwa Maadhimisho hayo kumeiwezesha Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kufanya tathmini ya namna ilivyotekeleza majukumu yake ya uratibu, usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi kwa kipindi cha miaka mitano tangu kuanzishwa kwake.

Ndani ya Toleo hili la Saba la Jarida la Wakili Mkuu, tunakuletea habari na makala maalum kuhusu mafanikio ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kipindi cha miaka mitano iliyopita tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018 hadi 2023. Ofisi hii imefanya kazi kwa bidii na uaminifu katika kutekeleza majukumu yake muhimu ya kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali hatua ambayo imeiwezesha Serikali kushinda mashauri mengi na hivyo kuokoa fedha.

Katika kipindi cha miaka mitano, Ofisi hii imedhihirisha umahiri wake katika kusimamia, kuratibu na kuendesha mashauri ya Serikali kwa ufanisi mkubwa hivyo kuwezesha kulinda maslahi mapana ya taifa. Kwa kuzingatia misingi ya utawala bora, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeweza kushirikiana na wadau wote katika kuwezesha kufikia azma ya Serikali ya kuleta maendeleo kwa wananchi wake na taifa kwa ujumla kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025.

Katika kipindi hicho, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeshirikiana na Wizara, Idara na Taasisi za Serikali katika uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ili kuwezesha utekelezaji wenye tija na ufanisi kwenye miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo ushauri katika kushughulikia migogoro kwenye ujenzi wa reli ya kisasa, bwawa la umeme la Mwalimu Nyerere, Daraja la Tanzanite, mashamba makubwa ya uwekezaji, masuala yanayohusisha kodi, ndege, katiba, haki za binadamu na uchaguzi.

Aidha, Ofisi hii imejenga ushirikiano thabiti na taasisi binafsi na za umma ikiwemo Wizara ya Katiba na Sheria, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Mahakama ya Tanzania, Mabaraza, na Wizara mbali mbali. Ushirikiano huu umeongeza ufanisi katika utendaji kazi na kuwezesha utoaji wa huduma bora kwa wadau na umma kwa ujumla ndani ya kipindi cha miaka mitano.

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa mashauri ya Serikali yanasimamiwa vyema kwa ufanisi na weledi wa hali juu kwa manufaa ya wananchi na taifa kwa ujumla ili kuendelea kuleta mafanikio makubwa zaidi na kuchangia katika ujenzi wa taifa letu.



**Prisca Jackson Ulomi**
**Mhariri Mkuu**

# Kutoka Kwenye Dawati la Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri



Sarah D. Mwaipopo
**Naibu Wakili Mkuu wa Serikali**

Toleo la Saba la Jarida la Wakili Mkuu wa Serikali ni maalumu kwa ajili ya kutathmini utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kutimiza miaka mitano tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018.

Katika kipindi cha miaka mitano, Ofisi inatambua mchango mkubwa wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan katka kuboresha Ofisi hii ili kuiwezesha kuwa mstari wa mbele katika kuunga mkono juhudi za Serikali kwa kuhakikisha inaiwakilisha vyema na kwa weledi mkubwa katika uratibu, usimamizi na uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi yaliyofunguliwa na au dhidi ya Serikali na taasisi zake ndani na nje ya nchi.

Aidha, napenda kuishukuru menejimenti na watumishi wote wa Ofisi hii chini ya uongozi wa Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Nalija Luhende kwa mchango wao mkubwa wa kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hii kwa kipindi cha miaka mitano tangu kuanzishwa kwake.

Kwa kuzingatia majukumu ya Ofisi hii, Toleo hili litajumuisha matukio muhimu yaliyofanyika katika kipindi cha Mwezi Aprili hadi Juni mwaka 2023 ikihusisha maadhimisho ya miaka mitano ya tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambapo Mgeni Rasmi kwenye Maadhimisho hayo alikuwa Waziri Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb).

Pia, Toleo hili litaangazia nafasi ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kukuza uchumi, mafunzo kwa Mawakili wa Serikali, maelekezo mahsusi yaliyotolewa na Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa taasisi mbalimbali za Serikali katika kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kutekeleza majukumu ya kuratibu, kuendesha na kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi ya ndani na nje ya nchi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake.

Pamoja na hayo, Toleo hili litagusia uteuzi uliofanywa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kumteua Bi. Irene Joseph Lesulie kuwa Naibu Kabidhi Wasii Mkuu wa RITA. Uteuzi huu unaipa heshima Ofisi hii kwa kuwa imekuwa ni Ofisi inayoendelea kuzalisha viongozi wanaoaminiwa na hatimaye kuteuliwa na kukasimiwa majukumu ya kuendesha baadhi ya taasisi za Serikali hivyo hatuna budi kuhakikisha tunaendelea kuwa kioo kwa taasisi nyingine na umma kwa ujumla kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za Serikali.

Vile vile, Toleo hili kwa upekee lina makala mbalimbali za kitaaluma zinazotokana na majukumu ya msingi ya Ofisi hii yenye lengo la kutoa elimu na kujenga uelewa kuhusu maamuzi mbalimbali pamoja na mahusiano ya Ofisi na taasisi nyingine. Pia, Ofisi inatambua na kushukuru mchango wa aliyekuwa Mkurugenzi wa Mipango, Dkt. Abdul Mussa Ally aliyefariki dunia kwa ajali ya gari tarehe 23 Aprili, 2023 akiwa safarini kikazi. Kipekee, napenda kuwashukuru menejimenti, watumishi wote wa Ofisi hii na wadau kwa kushiriki vyema katika kipindi cha maombolezo na mazishi. Mungu ailaze mahali pema peponi roho ya marehemu na apumzike kwa amani, Amen. Hakika sote ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea!.

Haya tu ni baadhi ya masuala mengi yatakayoakisiwa ndani ya Jarida hili. Naomba nimalizie kwa kuomba wasomaji wetu kuendelea kutoa maoni kwa Bodi ya Uhariri kwa ajili ya kuboresha Jarida hili ili kwa pamoja tuweze kulifanya Jarida hili kuendelea kutoa mchango chanya katika ukuaji wa Sekta ya Sheria hapa nchini. Nawatakia usomaji mwema wa Toleo la Saba la Jarida la Wakili Mkuu. Asanteni.

# Yaliyomo


| | |
|---|---|
| UK. 06 | Waziri Mkuu Mhe. Majaliwa Aipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Kuadhimisha Miaka Mitano tangu Kuanzishwa kwake |
| UK. 14 | Tumieni Mafunzo Kusimamia Vyema Mashauri ya Serikali |
| UK. 17 | Tumewanoa Mkapunguze Mlundikano wa Kesi Mahakamani |
| UK. 20 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yanunua Magari Mapya |
| UK. 25 | Bi. Mwaipopo: Hakuna Haki bila Uwajibikaji katika Utumishi wa Umma |
| UK. 29 | Baraza la Wafanyakazi Lapitisha Bajeti ya Shilingi Bilioni 17 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 |
| UK. 34 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yatengewa bajeti ya shilingi bilioni 17 |
| UK. 36 | Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Aongoza Watumishi Sherehe za Mei Mosi Kitaifa |
| UK. 41 | Mhe. Rais Dkt. Samia amteua Bi. Irene Joseph Lesulie kuwa Naibu Kabidhi Wasii Mkuu - RITA |
| UK. 42 | Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yalenga Kuboresha Mahusiano na Baraza la kimataifa la usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji (ICSID) |
| UK. 45 | Jaji mmoja ana mamlaka ya kusikiliza shauri la kikatiba lisilohusu haki za Binadamu |
| UK. 50 | Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo aliwaongoza watumishi wa OWMS kumuaga Dkt. Abdul Mussa Ally |



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), akionesha Jarida Maalum la Miaka Mitano ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mara baada ya kulizindua Dodoma. Kutoka kushoto ni Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb), Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi.*

# Waziri Mkuu Mhe. Majaliwa Aipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Kuadhimisha Miaka Mitano tangu Kuanzishwa kwake

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), aliipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuadhimisha miaka mitano tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018. Maadhimisho hayo yalijikita kwenye kauli mbiuisemayo,"MiakaMitano ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali: Tulipotoka, Tulipo na Tunapoelekea." Kauli mbiu hii inawawezesha kutathmini majukumu ya uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi kwa niaba ya Serikali na taasisi zake kwa umahiri mkubwa, weledi na kuisaidia Serikali kuokoa fedha ikiwa ni pamoja na kutatua migogoro kwa njia ya usuluhushi. Pia, aliipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuokoa zaidi ya shilingi trilioni saba kupitia mashauri yaliyoendeshwa na majadiliano.

Mhe. Majaliwa aliyasema hayo wakati akiwa Mgeni Rasmi kwenye Maadhimisho ya Miaka Mitano tangu kuanzishwa kwa Ofisi hiyo na uzinduzi wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete, jijini Dodoma ambapo alizielekeza Wizara, Idara na taasisi zote za Serikali kufanya kazi kwa karibu na Ofisi ya Wakili



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), akikata utepe kuzindua Jarida Maalum la Miaka Mitano ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Kutoka kushoto ni Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb), Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt Boniphace Luhende na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi.*

Mkuu wa Serikali katika uendeshaji wa mashauri hayo. Pia, amezitaka taasisi zote za umma zenye Mawakili wa Serikali kuzingatia suala la utatuzi wa kero za wananchi ili kupunguza mlundikano wa mashauri ambayo hayana ulazima wa kufikishwa mahakamani.

Akizungumza kabla ya kumkaribisha Mhe.

Majaliwa, Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb), alimueleza Mgeni Rasmi kuwa Wizara inaendelea na utekelezaji wa Kampeni ya Kitaifa ya Msaada wa Kisheria nchini kote ijulikanayo kwa jina la *"Mama Samia Legal Aid Campaign"* ili kutoa elimu kwa umma kuhusu masuala ya kisheria nchini kwa lengo la kupunguza mlundikano wa mashauri na migogoro mahakamani.

Kwa upande wake Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Mhe. Jaji Dkt. Eliezer Feleshi alisema kuwa uamuzi wa kuanzishwa kwa Ofisi hii ulilenga kuimarisha Sekta ya Sheria nchini hususani katika kuongeza ufanisi zaidi katika uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi nchini. Hatua hii imeiwezesha Serikali kuokoa fedha ambazo sasa zinaelekezwa katika kutekeleza miradi ya maendeleo nchini kwa manufaa ya taifa.

Kuhusu ushirikiano uliopo kati ya Ofisi yake na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Mhe. Yohane Massara, Jaji Kiongozi Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki alisema Ofisi yake itaendelea kutoa ushirikiano uliopo huku akitoa rai kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kuendelea kutoa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali sio tu yanayohusu uendeshaji wa mashauri ya madai na usuluhishi ya hapa nchini lakini pia mafunzo katika mahakama za kikanda na za kimataifa ili kuwe na



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) akipokea tuzo ya heshima kutoka kwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb) ya kutambua mchango wake katika kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kabla ya kufungua rasmi Maadhimisho ya Miaka Mitano ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali jijini Dodoma. Aliyesimama katikati akishuhudia ni Dkt. Boniphace Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akizungumza na Mawakili wa Serikali (hawapo pichani) wakati wa Maadhimisho ya Miaka Mitano ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na ufunguzi wa mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofanyika jijini Dodoma.*

muendelezo kwa Mawakili wengine katika kuitetea Serikali mara baada ya waliopo kustaafu.

Akitoa salamu za mkoa wa Dodoma na pongezi kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa utendaji mzuri, Mkuu wa Mkoa huo Mhe. Rosemary Senyamule alimpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa dhamira njema aliyonayo kwa kila sekta ikiwa ni pamoja na Sekta ya Sheria na taasisi zake katika kuhakikisha kuwa kila mwananchi anapata haki kwa wakati kupitia vyombo vya kisheria nchini.

Naye Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende alisema kuwa kauli mbiu ya Maadhimisho ya Miaka Mitano ya tangu kuanzishwa kwa Ofisi hiyo ni *"Miaka Mitano ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali: Tulipotoka, Tulipo na Tunapoelekea"*, yenye lengo la kufanya tathmini ya namna inavyotekeleza majukumu yake kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ili kuboresha utendaji kazi kama ilivyokasimiwa na Serikali.

Dkt. Luhende aliongeza kuwa hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2023, Ofisi imeendesha jumla ya mashauri 7,162 ikiwemo mashauri 7,025 ya madai na mashauri 137 ya usuluhishi.

Baadhi ya mafanikio yaliyopatikana kwa kipindi cha miaka mitano tangu kuanzishwa kwake ni kama ifuatavyo: usimamizi wa mashauri ya madai na usuluhishi ambapo hadi kufikia tarehe 31 Mei, 2023; Ofisi imeendesha jumla ya mashauri 7,162 ikiwemo mashauri 7,025 ya madai na mashauri 137 ya usuluhishi.

Dkt. Luhende anafafanua kuwa katika kipindi cha Mwaka wa fedha 2022/2023 hadi Aprili 30, 2023; Ofisi ilimaliza mashauri ya madai 518 kati ya mashauri hayo mashauri 45 yaliisha kwa njia ya majadiliano. Ofisi pia ilimaliza mashauri ya



*Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akimsikiliza Mkurugenzi Msaidizi Udhibiti Ubora wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Mercy Kyamba alipotembelea banda la Ofisi hiyo wakati wa Maadhimisho ya Miaka Mitano ya Ofisi hiyo na uzinduzi wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Dodoma.*

usuluhishi kumi na tano (15) kati ya mashauri hayo 6 yaliisha kwa majadiliano. Hivyo, kuokoa shilingi bilioni 305.41 kwa mashauri ya madai na shilingi trilioni 7.26 kwa mashauri ya usuluhishi na kufanya fedha zote zilizookolewa kuwa jumla ya shilingi trilioni 7.57.

Vilevile, Ofisi imeongoza na kushiriki katika Timu za Serikali za Majadiliano (Government Negotiation Team) na kufanikisha kumaliza mashauri/ migogoro mbalimbali kwa njia ya majadiliano, usuluhishi na maridhiano nje ya Mahakama kwa mafanikio makubwa.

Mafanikio mengine ni kuimarisha Mifumo ya Usimamizi wa mashauri na Udhibiti wa Ubora. Katika kipindi cha miaka mitano, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, imeimarisha mfumo wa kukusanya takwimu za mashauri, kufanya ufuatiliaji wa mienendo ya mashauri na kupitia sheria zinazohusu mashauri ya madai na usuluhishi.

Aidha, Ofisi imeweza kuandaa Miongozo ya kusimamia na kudhibiti viwango vya ubora vya Mawakili wa Serikali katika uendeshaji wa mashauri (Civil Litigation and Arbitration Practice Directions, 2021 and Quality Assurance Manual, 2021). Vile vile, Ofisi imeweza uandaa Mkataba wa Huduma kwa Mteja (Client Service Charter) ambao unaiwezesha Ofisi ya Wakili Mkuu kuweka aina ya huduma, viwango, ubora, haki na wajibu wa mteja na utaratibu unaotumika kutoa huduma kwa wadau ikiwemo Serikali na taasisi zake, sekta binafsi na wananchi na namna ya kupata mrejesho.

“Tunaishukuru Serikali kwa kuendelea kuongeza bajeti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi ilipata bajeti ya shilingi bilioni 4.17; shilingi bilioni 7.29 kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020; shilingi bilioni 11.48 kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; shilingi bilioni 12.13 kwa Mwaka wa Fedha 2021/22; shilingi billioni 12.81 kwa Mwaka wa Fedha 2022/23; na kwa Mwaka wa Fedha 2023/24; Ofisi imepatiwa bajeti ya shilingi billioni 17.07 sawa na ongezeko la asilimia 25

ukilinganisha na bajeti ya Mwaka wa Fedha 2022/23,” anasema Dkt. Luhende.



*Mkuu wa Mkoa wa  Dodoma, Mhe. Rosemary Senyamule akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Miaka Mitano ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na uzinduzi wa mafunzo kwa Mawakili yaliyofanyika jijini Dodoma.*

Kuongezeka kwa bajeti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kumeiwezesha Ofisi kutekeleza majukumu yake ya msingi ya usimamizi na uendeshaji mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali kwa ufanisi na kupunguza changamoto zinazotokana na ufinyu wa bajeti uliokuwepo hapo awali.

Aidha, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2022/2023 hadi Aprili 30, 2023; Ofisi ilimaliza mashauri ya madai 518 kati ya mashauri hayo mashauri 45 yaliisha kwa njia ya majadiliano. Ofisi pia ilimaliza mashauri ya usuluhishi kumi na tano



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akizungumza na Mawakili wa Serikali (hawapo pichani) wakati wa Maadhimisho ya Miaka Mitano ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na ufunguzi wa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika jijini Dodoma.*



*Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Dkt. Joseph Mhagama akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Miaka Mitano ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na uzinduzi wa mafunzo kwa Mawakili yaliyofanyika jijini Dodoma.*

(15) kati ya mashauri hayo 6 yaliisha kwa majadiliano.

Akitambulisha viongozi, wageni waalikwa na wadau, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo alisema kuwa sambamba na maadhimisho hayo ya miaka mitano, Ofisi ililenga kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali katika masuala mbali mbali ya kisheria ikiwemo uandaaji wa mikataba ya uwekezaji, mafuta na gesi, uwekezaji na uendeshaji wa migogoro nje ya mahakama.

Ndugu Tumaini Kweka, Mwakilishi wa Mkurugenzi wa Taifa wa Mashtaka alisema kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imekuwa na ushirikiano mkubwa na wanufaika wa uwepo wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali hasa katika uendeshaji wa mashauri mbali mbali ya madai yanayotokana na kesi za jinai ambazo zimefunguliwa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mahakama ya Rufaa na Mahakama ya Haki ya Afrika Mashariki.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria, Dkt. Joseph Mhagama akimwakilisha Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alieleza kuwa Bunge kwa kutambua majukumu ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliiongezea bajeti kufikia shilingi bilioni 17 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Prof. Elisante Ole Gabriel alibainisha kuwa Mahakama inafanya maamuzi yake kwa kutegemea ushirikiano unaotolewa na Mawakili wa Serikali kwa niaba ya Serikali. Pia, Mahakama imekuwa na ushirikiano mkubwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati.

Mwakilishi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Bi. Fatuma Idd alimueleza Mgeni Rasmi kuwa mwaliko huu unadhihirisha ushirikiano uliopo baina ya taasisi zetu ambapo sote kwa pamoja tunashirikiana kuiwakilisha Serikali katika mashauri ya madai na usuluhishi ndani na nje ya nchi na kwenye mafunzo kwa lengo la kuongeza ujuzi na weledi kwa Mawakili ili kuendana na kasi ya mabadiliko yanayoakisi kazi na majukumu yetu ya kila siku.



*Mtendaji Mkuu wa Mahakama ya Tanzania, Prof. Elisante Ole Gabriel akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Miaka Mitano ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na uzinduzi wa mafunzo kwa Mawakili yaliyofanyika jijini Dodoma.*



*Jaji Kiongozi wa Mahakama ya Haki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki, Mhe. Yohane Massara akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Miaka Mitano ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na uzinduzi wa mafunzo kwa Mawakili yaliyofanyika jijini Dodoma.*



*Mwakilishi wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Bi. Fatuma Idd akizungumza wakati wa Maadhimisho ya Miaka Mitano ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na uzinduzi wa mafunzo kwa Mawakili yaliyofanyika jijini Dodoma.*



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akizungumza na Mawakili wa Serikali (hawapo pichani) walioshiriki mafunzo ya kuwajengea uwezo katika masuala ya kisheria ikiwemo uandaaji wa mikataba ya uwekezaji, miradi inayohusu mafuta na gesi. Mafunzo hayo ya siku tatu yalifanyika jijini Dodoma.*

# Tumieni Mafunzo Kusimamia Vyema Mashauri ya Serikali

Mawakili wa Serikali kutoka Wizara, taasisi, Idara za Serikali, mikoa na Halmashauri zote nchini wametakiwa kutumia mafunzo waliyopata ili waweze kusimamia vyema mashauri ya Serikali katika Mahakama mbalimbali ndani na nje ya nchi.

Wito huo ulitolewa na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende wakati akitoa neno

la ukaribisho kwa Mawakili wa Serikali walioshiriki mafunzo hayo ya siku tatu yaliyofanyika kwenye ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

Akizungumza kuhusu mafunzo hayo, Dkt. Luhende alisema kuwa lengo kubwa la mafunzo haya kwa Mawakili wa Serikali pamoja na mambo mengine yalilenga kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali katika masuala mbalimbali ili kuongeza ufanisi kwenye utekelezaji wa majukumu yao kwa weledi zaidi.

Dkt. Luhende aliongeza kuwa mafunzo haya yanahusisha masuala mbalimbali ya sheria ikiwemo uandaaji na usimamizi wa mikataba, mafuta na gesi, masuala ya uwekezaji na usuluhushi wa migogoro kwa njia ya majadiliano.

Aidha, alieleza kuwa kauli mbiu ya mafunzo hayo ililenga kuwafanya Mawakili wa Serikali kuwa chachu ya kuzuia, kupunguza na kumaliza migogoro kwa njia ya majadiliano kwa kuzingatia kuwa Serikali kupitia Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanya juhudi za makusudi kuvutia wawekezaji ili kukuza uchumi wa nchi yetu.

Alisisitiza kuwa ili wawekezaji wavutiwe kuja ni lazima tuwe na mifumo imara na thabiti ya kutatua migogoro kwa kutumia njia mbadala kama vile usuluhishi, majadiliano na maridhiano. Njia hizi huokoa muda, hupunguza gharama na huboresha mahusiano kati ya nchi na wawekezaji au wadau wengine wa Serikali pale inapojitokeza migogoro.

Aidha, aliongeza kuwa maeneo mengine yatakayoguswa na mafunzo hayo ni njia na taratibu za kutatua migogogro ya manunuzi na matumizi ya akili bandia (artificial intelligence) katika kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi. Pamoja na masuala ya kisheria, maeneo hayo ni muhimu kwa Mawakili wa Serikali ili kuhakikisha wakati wote kazi za Serikali zinafanyika kwa umakini na weledi wa hali ya juu.

Vile vile, watapata wasaa wa kujifunza namna bora ya kuondoa vikwazo na sintofahamu zinazosababishwa kwa kukiuka taratibu za manunuzi kwa mujibu wa



*Baadhi ya washiriki wakifuatilia mada mbalimbali zilizotolewa kwa Mawakili wa Serikali wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo katika masuala ya kisheria ikiwemo uandaaji wa mikataba ya uwekezaji na miradi inayohusu mafuta na gesi. Mafunzo hayo ya siku tatu yamefanyika kwenye ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.*

sheria ya manunuzi, kanuni, miongozo na desturi za kutekeleza majukumu ya Serikali.

Kwa upande wake Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akizungumza wakati akimkaribisha Dkt. Luhende alisema kuwa mafunzo hayo ni mwendelezo wa mipango ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali katika kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Mawakili wa Serikali waliopewa hati idhini ya kuendesha mashauri ya Serikali kwa niaba ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Mafunzo haya yaliratibiwa na kuendeshwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yanahusisha washiriki zaidi ya mia sita kutoka Wizara, taasisi, Idara, Mikoa na Halmashauri zote nchini na kuhusisha wakufunzi wabobezi wakiwemo Majaji na Majaji wastaafu kutoka Mahakama Kuu ya Tanzania na wakufunzi kutoka vyuo mbali mbali nchini.



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sara Mwaipopo akizungumza na Mawakili wa Serikali wanaoshiriki mafunzo ya kuwajengea uwezo katika masuala ya kisheria ikiwemo uandaaji wa mikataba ya uwekezaji na miradi inayohusu mafuta na gesi. Mafunzo hayo ya siku tatu yamefanyika kwenye ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.*



*Baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (walioketi mbele) wakifuatilia mada mbalimbali zilizotolewa kwa Mawakili wa Serikali wakati wa mafunzo ya kuwajengea uwezo katika masuala ya kisheria ikiwemo uandaaji wa mikataba ya uwekezaji na miradi inayohusu mafuta na gesi. Mafunzo hayo ya siku tatu yamefanyika kwenye ukumbi wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.*

# Tumewanoa Mkapunguze Mlundikano wa Kesi Mahakamani



*Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo, akizungumza na Mawakili wa Serikali wakati akifunga mafunzo ya siku tatu kwa Mawakili wa Serikali yaliyofanyika katika ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma.*

Serikali imewanoa Mawakili wa Serikali ili wakapunguze mlundikano wa kesi mahakamani. Hayo yalisemwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Bi. Mary Makondo wakati akifunga mafunzo kwa Mawakili wa Serikali yaliyotolewa kwa siku tatu kwenye ukumbi wa mikutano wa Jakaya Kikwete jijini Dodoma.

Bi. Makondo aliwaambia Mawakili hao kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeratibu na kufadhili mafunzo kwa Mawakili wa Wizara, taasisi, Idara na Halmashauri zote nchini yaliyogusa maeneo mbali mbali ikiwemo utatuzi wa migogoro, masuala ya ufilisi, uamuzi na usuluhishi wa kitaifa na kimataifa, mbinu za kuzuia migogoro, mikataba ya uwekezaji, afya ya akili, matumizi ya TEHAMA na akili bandia katika uendeshaji wa mashauri.

Aliongeza kuwa Serikali imewanoa Mawakili hao ili wakasaidie kupunguza migogoro katika maeneo mbalimbali, na hivyo kuwezesha ufanisi kwenye utekelezaji wa mikataba na shughuli nyingine za kiuchumi.

Aidha, aliwataka Mawakili wote wa Serikali kuzingatia maelekezo yaliyotolewa na Mhe. Kassim Majaliwa



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akizungumza na Mawakili wa Serikali wakati akimkaribisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Bi. Mary Makondo (hayupo pichani) ili aweze kufunga mafunzo kwa Mawakili hao yaliyofanyika Jijini Dodoma.*




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akizungumza na Mawakili wa Serikali wakati akimkaribisha Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende ( hayupo pichani) wakati wa kufunga mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kutoka kwenye Wizara, taasisi, Idara, Mikoa na Halmashauri zote nchini yaliyofanyika Jijini Dodoma.*

Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akifungua Maadhimisho ya Miaka Mitano tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na mafunzo kwa Mawakili wa Serikali.

Vile vile, aliipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kufanya maadhimisho yaliyotoa fursa ya kufanya tathmini ya utekelezaji wa majukumu kwa lengo la kuboresha utendaji kazi kwa manufaa ya umma.

Akizungumza wakati akimkaribisha Mgeni Rasmi, Bi. Makondo kufunga mafunzo hayo, Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende alisema kuwa Ofisi inashukuru kwa ushirikiano iliyopata kutoka Wizara , Idara, taasisi za Serikali na Halmashauri zote nchini kwa kuridhia na kuwawezesha Mawakili wa Serikali kushiriki mafunzo hayo.

Naye Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo aliwashukuru wafadhili na wadau mbalimbali waliowezesha mafunzo hayo kwa takribani Mawakili 600 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar kwa siku tatu mfululizo.

Akizungumza kwa niaba ya Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Bi. Fatuma Idd alishukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuialika Afisi hiyo kushiriki katika mafunzo hayo yenye lengo la kuwasaidia Mawakili wa Serikali katika utendaji kazi wao.

Pia, aliwapongeza na kuwashukuru watoa mada walioendesha mafunzo na Mawakili kwa kushiriki mafunzo hayo.

Ndugu Elias Mawera wa TARURA alishukuru Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa mafunzo kwa niaba ya washiriki wengine. Kwa kupitia mafunzo hayo, Mawakili wa Serikali wamepata nafasi ya kujifunza mbinu mpya na kubadilishana uzoefu wa uendeshaji wa Mashauri.




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akimshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Bi. Mary Makondo baada ya kufunga mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kutoka Wizara, taasisi, Idara, Mikoa na Halmashauri zote nchini. Mafunzo hayo yaliratibiwa na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.*




# *Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali Yanunua Magari Mapya*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imenunua na kukabidhi magari mapya 10 kwenye Ofisi zake zilizopo kwenye mikoa 10 kati ya mikoa 16 nchini zenye Ofisi hiyo ili kuwawezesha Mawakili Wafawidhi na Mawakili wa Serikali wa Ofisi hiyo kutekeleza majukumu yao ipasavyo kwa niaba ya Serikali na taasisi zake ya kuendesha na kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali.

Magari hayo yalikabidhiwa na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende, kwa Mawakili Wafawidhi wakati wa mkutano mkuu wa watumishi wa Ofisi hiyo uliofanyika jijini Dodoma.

Akikabidhi magari hayo, Dkt. Luhende amewataka Mawakili hao kutumia magari hayo kuongeza ari, chachu na ufanisi katika kusimamia na kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi kwa niaba ya Serikali kwenye mikoa wanakotekeleza majukumu yao.

"Natambua mchango wa Mawakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali waliopo kwenye Ofisi za mikoa 16 ambako mnatekeleza majukumu yenu, mtambue kuwa Ofisi hii imeaminiwa na Serikali na taasisi zake kwa niaba ya Serikali kuendesha na kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi. Hivyo, tuelewe kuwa tunawajibika kwa umma ili fedha za Serikali tunazookoa kwa kushinda mashauri zitumike kuleta maendeleo ya nchi yetu," alisema Dkt. Luhende.

Naye Naibu Wakili Mkuu wa



*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (aliyesimama katikati) akikata utepe kwa ajili ya kukabidhi magari mapya 10 ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Mawakili Wafawidhi wa Mikoa. Kushoto ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo na kulia Wakili wa Serikali Mfawidhi Ofisi hiyo Mkoa wa Rukwa, ndugu Mujahidi Kamugisha.*

Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akishuhudia makabidhiano ya magari hayo alisema kuwa hadi sasa Ofisi zote za Wakili Mkuu wa Serikali zilizopo kwenye mikoa 16 zimepata magari hayo. Hivyo, aliwataka Mawakili hao waliopo kwenye mikoa hiyo kutumia vizuri magari hayo na kuyatunza ili waweze kuendesha Mashauri yaliyopo kwenye maeneo ya kijiografia ya mikoa wanayofanyia kazi ili kusogeza huduma karibu.

"Magari hayo mapya 10 yatatumika kutoa huduma kwenye mikoa ya Shinyanga, Mtwara, Morogoro, Rukwa,




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akikabidhi kadi ya gari kwa Wakili wa Serikali wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wa Mkoa wa Shinyanga, ndugu Mussa Mpogole wakati wa makabidhiano ya magari hayo jijini Dodoma.*





*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akikabidhi kadi ya gari kwa Wakili Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wa Mkoa wa Kagera, ndugu Gerald Njoka wakati wa makabidhiano wa magari hayo jijini Dodoma.*

Kagera, Ruvuma, Tanga, Mara, Kilimanjaro na Iringa ambapo awali tayari magari 6 yalikabidhiwa kwenye mikoa 6 ya Arusha, Kigoma, Dodoma, Mbeya, Tabora na Mwanza. Hivyo, kuifanya kila Ofisi iliyopo mkoani kuwa na gari," alifafanua Bi. Mwaipopo.

Pia, ameongeza kuwa Ofisi ina utaratibu wa kuwa na mkutano mkuu wa watumishi wa Ofisi kila mwaka kwa lengo la kufanya tathmini ya utekelezaji wa majukumu waliyopanga kuyatekeleza ili kuweza kujadiliana na kupeana taarifa ili kuboresha utendaji kazi kwa maslahi mapana ya taifa.

Akisoma taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 kwenye mkutano huo; Bi. Mwaipopo alisema Ofisi imetekeleza majukumu mbali mbali kwa ufanisi ikiwemo kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu Dodoma,kufanya mapitio ya muundo wa kiutumishi wa Ofisi hiyo ili kuboresha maslahi ya watumishi, kuongeza idadi ya watumishi wapya, kuwawezesha watumishi kupata mafunzo ya muda mfupi na mrefu ndani na nje ya nchi.,kuboresha mazingira ya kufanyia kazi na ununuzi wa vitendea kazi.

Mkutano huo ulihudhuriwa na watumishi wa kada mbali mbali kutoka kwenye Ofisi 17 za Wakili Mkuu wa Serikali zilizopo kwenye mikoa mbalimbali nchini.



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akimkabidhi kadi ya gari Wakili Mfawidhi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wa Mkoa wa Mtwara, ndugu Masunga Kamihanda wakati wa makabidhiano ya magari hayo jijini Dodoma.*




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (aliyeketi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Mawakili Wafawidhi wa Mikoa wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali mara baada ya kufungua mkutano mkuu wa Ofisi hiyo uliofanyika Jijini Dodoma. Wapili kutoka kushoto ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo*




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (aliyeketi watatu kutoka kulia) akiwa kwenye picha ya pamoja na Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali walioshiriki mkutano mkuu wa Ofisi hiyo uliofanyika Jijini Dodoma. Watatu kutoka kushoto ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo*




*Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (aliyeketi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kutoka Kitengo cha Masijala ya Sheria na Kitengo cha Huduma za Maktaba na Utafiti mara baada ya kufungua mkutano mkuu wa Ofisi hiyo uliofanyika jijini Dodoma. Wapili kutoka kushoto ni Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo*



**Bi. Sarah D. Mwaipopo**

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali

# *Bi. Mwaipopo: Hakuna Haki bila Uwajibikaji katika Utumishi wa Umma*

Watumishi wapya kutoka Ofisi ya Wakili Mkuu Mkuu wa Serikali wametakiwa kuwajibika ipasavyo katika kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa weledi kwa kuwa hakuna haki bila uwajibikaji katika utumishi wa umma.

Hayo yalisemwa tarehe 4 Mei, 2023 na Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo wakati akifungua mafunzo elekezi kwa watumishi wapya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS). Mafunzo hayo yalikuwa na lengo la kuwajengea uwezo watumishi hao kuhusu masuala

mbalimbali ya kiutumishi ikiwemo kufanyakazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

Akizungumzia aina ya mafunzo yatakayotolewa, Bi. Mwaipopo alisema kuwa Ofisi hiyo imekusudia kuwajengea uwezo watumishi hao katika masuala mbalimbali yanayohusu majukumu yao, haki na wajibu wa watumishi wa umma, muundo wa Serikali, taratibu za utendaji kazi, maadili, nidhamu, uadilifu na ustahimilivu ambavyo vyote kwa pamoja vinapaswa kuzingatiwa ili kuimarisha utendaji kazi kwa watumishi wa umma hususan kwa ajira mpya.

Alieleza kuwa mafunzo hayo ni utekelezaji wa matakwa ya kisheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma ambapo Ofisi imeona umuhimu wa kutenga bajeti ili kufanikisha mafunzo haya muhimu yatakayowajenga na kuwapa uelewa katika masuala mbalimbali ya kiutumishi.

Akizungumzia umuhimu wa mafunzo hayo, Bi. Mwaipopo aliwaeleza kuwa mafunzo hayo yatawasaidia katika kuimarisha utendaji kazi, nidhamu na maadili ikiwa ni pamoja kuwawezesha kuepuka makosa mbalimbali ya kinidhamu na yale ya kiutumishi ambayo yangeweza kufanyika kwa kukosa uelewa ili kuweza kuyaepuka wakiwa mahali pa kazi.

Naye Wakili wa Serikali, Francis Oswald aliishukuru Ofisi kwa kuandaa mafunzo hayo muhimu ambayo yatawawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi kwa kuzingatia maadili ya utumishi wa umma.

Mafunzo hayo ya siku mbili yaliwahusisha watumishi 64 waajiriwa wapya wa Ofisi hiyo wa kada mbali mbali ikiwemo Mawakili wa Serikali arobaini na moja, Maafisa TEHAMA wawili, Makatibu Sheria wanne, Katibu Muhtasi watatu, Madereva tisa, Watunza Kumbukumbu wanne na Afisa Usafirishaji mmoja.



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo (aliyeketi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na waajiriwa wapya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali baada ya kufungua mafuzo elekezi kwa watumishi hao yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani. Wa pili kulia ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, ndugu James Kibamba wa Ofisi hiyo.*



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akisaini kitabu cha wageni alipowasili katika Chuo cha Uongozi cha Mwalimu Nyerere, Kibaha kwa ajili ya kufungua mafunzo elekezi ya siku mbili kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.*




*Waajiriwa wapya wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza kwa makini Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (hayupo pichani) wakati akifungua mafunzo elekezi kuhusu sheria, taratibu na kanuni za utumishi wa umma yaliyofanyika Kibaha Mkoani Pwani.*



*Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, ndugu James Kibamba akimkaribisha Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (hayupo pichani) kufungua mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya wa Ofisi hiyo yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*




*Baadhi ya wajumbe wa Menejimenti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakimsikiliza kwa makini Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo (hayupo pichani) wakati akifungua mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya (hawapo pichani) wa Ofisi hiyo yaliyofanyika Kibaha mkoani Pwani.*




# *Baraza la Wafanyakazi Lapitisha Bajeti ya Shilingi Bilioni 17 kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024*

*Wakili Mkuu wa Serikali na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (aliyeketi katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi mara baada ya kufungua Kikao cha Pili cha Baraza la pili la Wafanyakazi kilichofanyika mkoani Morogoro.*

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali (OWMS) kwa kushirikiana na Timu ya Taifa ya usuluhishi imefanikiwa kuokoa kiasi cha shilingi trilioni 7.170 baada ya kumaliza majadiliano ya mashauri ya usuluhishi yaliyofunguliwa dhidi ya Serikali ya Tanzania nje ya nchi.

Kauli hiyo imetolewa na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt Boniphace Luhende kwenye kikao cha Pili cha Baraza la pili la Wafanyakazi Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kilichofanyika mkoani Morogoro.

Alisema kuwa kiasi hicho cha fedha kilichookolewa ni kile ambacho kingelipwa iwapo Serikali ingeshindwa mashauri ya usuluhishi yaliyofunguliwa dhidi yake katika Mahakama ya usuluhishi ya jijini London na Baraza la Kimataifa la usuluhishi wa Migogoro ya Kibiashara (ICC).

“Ofisi yetu iliweza pia kuiwakilisha vyema Serikali katika kutetea migogoro inayohusu miradi mikubwa ya Serikali kwa kuhakikisha kuwa miradi hiyo inaendeshwa kwa ufanisi mkubwa kwa kufuata sheria na bila ya vikwazo mbalimbali,“ alisema Dkt. Luhende

Alisema kuwa OWMS katika kipindi cha miaka miwili ya Serikali ya Awamu ya Sita imefanikiwa kuiwakilisha Serikali kwa ufanisi katika mashauri yote ya madai na usuluhishi kwa kuendesha jumla ya mashauri 6,263 ikiwemo mashauri 6,112 ya madai na mashauri 151 ya usuluhishi.

Ameongeza kuwa OWMS inachangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi kwa kushiriki katika utatuzi wa haraka wa migogoro inayohusu Serikali na washitiri wake, Serikali na wananchi au taasisi ili kuziwezesha pande husika kuendelea na shughuli za maendeleo.

Aidha, Dkt Luhende aliishukuru Serikali




*Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakifuatilia mada mbalimbali zinazotolewa wakati wa Kikao cha Pili cha Baraza la Pili la Wafanyakazi kilichofanyika mkoani Morogoro.*

ya Awamu ya Sita (6) inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi inavyowezesha kwa hali na mali na ambavyo inatoa kipaumbele kwa mahitaji ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

"Katika kipindi cha Awamu ya Sita ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali iliongezewa bajeti yake kutoka shilingi bilioni 11.48 kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 hadi kufikia ukomo wa kiasi cha shilingi bilioni 17,075,830,000.00. kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024", alisema Dkt. Luhende.

Awali akitoa neno la ukaribisho, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo alisema madhumuni ya mkutano huo ni kuwawezesha wafanyakazi kupitia Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ili kuwa na uelewa wa pamoja kuhusu masuala ya Bajeti ya OWMS.

Bi Mwaipopo alisema kuwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 OWMS imejiwekea malengo nane (8) tofauti na Mwaka wa Fedha 2022/23 uliokuwa na malengo sita (6) ambapo malengo mawili yaliyoongezeka ni malengo mtambuka ambayo yanahusu masuala ya mazingira na lishe ambapo Serikali imeelekeza Wizara, taasisi za Serikali na Serikali za Mitaa kutenga kwenye bajeti.

"Vipaumbele vya bajeti yetu kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 ni kuendelea kuratibu, kusimamia na kuiwakilisha Serikali na taasisi zake katika kuendesha mashauri ya madai na usuluhishi yaliyofunguliwa dhidi ya Serikali au na Serikali katika Mahakama na Mabaraza mbalimbali ndani na nje ya nchi na masuala ya udhibiti ubora", alisema Bi. Mwaipopo

Aliongeza kuwa vipaumbele vingine ni kuendelea na ujenzi wa makao makuu ya Ofisi jijini Dodoma, kuimarisha Ofisi za mikoani, kuwajengea uwezo watumishi, kuimarisha mifumo ya TEHAMA ikiwa ni pamoja na kuboresha mfumo wa usimamizi wa mashauri na kuboresha mazingira ya utendaji kazi.

Mkutano huo wa Baraza la Wafanyakazi uliofanyika kwa siku mbili, ambapo katika siku ya kwanza ya Mkutano huo, wajumbe walipatiwa mafunzo kuhusu umuhimu





*Baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakifuatilia mada mbalimbali zinazotolewa wakati wa Kikao cha Pili cha Baraza la Pili la Wafanyakazi kilichofanyika mkoani Morogoro.*

wa usalama mahala pa kazi; haki na wajibu katika utumishi wa umma na elimu juu ya afya ya akili. Katika siku ya pili ya mkutano, wajumbe walipitisha makadirio ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024; walipokea rasimu ya Mwongozo wa Kurudisha kwa Jamii; na walipitia taarifa ya Maboresha ya Mfuko wa Kusaidiana. Vilevile, wajumbe walipokea ufafanuzi kutoka kwa Menejimenti ya Ofisi kuhusu Uboreshaji wa Muundo wa Utumishi; Upandaji wa madaraja; na Mpango wa mafunzo kwa watumishi.



*Wakili Mkuu wa Serikali na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akizungumza na wajumbe wa Baraza la wafanyakazi (hawapo pichani) wakati akifungua kikao cha Pili cha Baraza hilo kilichofanyika mkoani Morogoro.*

Naye mjumbe wa Baraza la Wafanyakazi, Motte Eliud aliupongeza uongozi wa OWMS kwa kuwapa nafasi wajumbe kupitia bajeti ya Ofisi na kupata fursa ya kuelewa mipango ya Ofisi kwa mwaka ujao wa fedha.

"Kwa sasa tumeshajua uelekeo na mpango wa Ofisi tunaahidi kuwa tutajitahidi kwa kadri ya uwezo wetu kuhakikisha tunatekeleza majukumu yetu na kufikia matarajio ya Ofisi na ya Serikali," alisema Motte.




*Katibu wa Baraza la Wafanyakazi la Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Zuhura Kussaga akitoa ufafanuzi kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakati wa Kikao cha Pili cha Baraza la pili la Wafanyakazi kilichofanyika mkoani Morogoro.*




*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali na Makamu Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi, Bi. Sarah Mwaipopo akizungumza na wajumbe wa Baraza hilo (hawapo pichani) wakati akimkaribisha Mwenyekiti wa baraza hilo (hayupo pichani) ili aweze kufungua kikao cha Pili cha Baraza la pili la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kilichofanyika mkoani Morogoro.*




*Wakili Mkuu wa Serikali na Mwenyekiti wa Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende (aliyeketi katikati) akiwa kwenye picha ya pamoja na wajumbe wa Baraza hilo wanaowakilisha Ofisi za mikoani muda mfupi baada ya kufungua kikao cha Pili cha Baraza hilo kinachofanyika mkoani Morogoro.*

# *Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yatengewa bajeti ya shilingi bilioni 17*



**Mhe. Dkt. Tulia Ackson**
**Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**



**Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb)**
**Waziri wa Katiba na Sheria**

Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2023/24 imefanikiwa kutengewa bajeti ya shilingi bilioni 17 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake ya kila siku.

Hayo yamezungumzwa na Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb), wakati akiwasilisha Bungeni Mpango na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024.

Akizungumza wakati wa kuwasilisha bajeti hiyo, Mhe. Dkt. Ndumbaro (Mb), aliipongeza Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuiongezea bajeti Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali

hatua itakayoiwezesha Ofisi hiyo kuendelea kusimamia mashauri ya madai na usuluhishi kwa ufanisi na weledi zaidi.

Ameongeza kuwa fedha hizo zilizotengwa kwa ajili ya uendeshaji wa Ofisi zitasaidia kwa kiasi kikubwa kuhakikisha utekelezaji wa majukumu unafanyika kwa wakati na ufanisi zaidi ikiwa ni pamoja na kuwezesha ulipaji wa mishahara kwa watumishi pamoja na kuwezesha gharama za matumizi mengineyo zitakazosaidia utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya Ofisi.

Pia ameipongeza Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa kuendelea kuiwakilisha vyema Serikali sambamba na kuiongoza na kushiriki katika Timu za Serikali za Majadiliano (GNT) ambazo zinaundwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, na kufanikisha kumaliza mashauri/ migogoro mbalimbali kwa njia ya majadiliano, usuluhishi, na maridhiano nje ya Mahakama. Utaratibu huu umeweza kuvutia wawekezaji nchini kwa kumaliza mapema migogoro mbalimbali dhidi ya wawekezaji na wafanyabiashara kwa njia ya majadiliano.

Alifafanua kuwa uendeshaji mashauri kwa njia ya usuluhishi na majadiliano umeisaidia Serikali kuokoa fedha ambazo zingetumika katika kuendesha migogoro tajwa zinazojumuisha gharama za usafiri, posho kwa Mawakili wa Serikali na mashahidi na ada za mahakama, kudumisha uhusiano kati ya Serikali na wawekezaji, kujenga imani kwa wawekezaji kuhusu hali ya utoaji haki nchini, pamoja na kukuza diplomasia ya uchumi ndani na nje ya nchi.

Kuhusu usuluhishi wa migogoro ya kibiashara, Sheria za kimataifa na Mikataba Mhe. Dkt. Ndumbaro alisema kuwa katika kipindi cha Julai 2022 hadi Machi 2023, Wizara kwa kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ilifanya mapitio ya sheria ya usuluhishi na kuandaa mapendekezo ya uboreshwaji wa sheria hiyo kwa kukusanya maoni ya wadau kuhusu mapendekezo ya maboresho na kuandaa rasimu ya marekebisho ya sheria hiyo kwa madhumuni ya kuimarisha mfumo wa usuluhishi wa migogoro ya kibiashara nchini.

Vile vile, Wizara kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imeandaa miongozo ya mafunzo ya usuluhishi, Upatanishi, Uendeshaji maridhiano na majadiliano itakayotumika kufundishia Wasuluhishi, Wapatanishi, Waendesha Maridhiano na Majadiliano pamoja na mwongozo wa kuendesha vikao vya Jopo la Ithibati la Waendesha Usuluhishi, Upatanishi, Majadiliano na Maridhiano.

Pia uwasilishaji wa hotuba ya Waziri Wa Katiba Na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (Mb), Bungeni ilihusisha pia Makadirio ya Mapato Na Matumizi ya taasisi zote zilizopo chini ya Wizara ya Katiba na Sheria ambazo ni Mahakama ya Tanzania, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Mastaka, Shule ya Sheria kwa Vitendo, Chuo cha Uongozi wa Mahakama, Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini, Tume ya Utumishi wa Mahakama, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala na Utawala Bora na Tume ya Kurekebisha Sheria.

***Shilingi bilioni 17***




Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan
**Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**

# *Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Aongoza Watumishi Sherehe za Mei Mosi Kitaifa*

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo aliwaongoza watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, kushiriki Maadhimisho ya kilele cha Siku ya Wafanyakazi Duniani (Mei Mosi) ambapo mgeni rasmi alikuwa Rais wa Jamhuri ya Muungao Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Akizungumza wakati wa Kilele cha Maadhimisho hayo, Mgeni Rasmi Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alisema kuwa Siku ya Wafanyakazi Duniani ni siku ya kutambua mchango wao katika kukuza uchumi na ustawi wa taifa letu.

Aidha, aliongeza kuwa hii ni siku ya kutoa shukrani kwa wafanyakazi nchini kwa kazi kubwa wanayoifanya ndani ya taifa letu kwa kujitoa kwao na kufanya kazi

kwa bidii kumesaidia kwa kiasi kikubwa kujenga taifa linalojitambua.

Aliongeza kuwa kama wafanyakazi lazima tujipongeze kwa kuwa umadhubuti wa taifa hili unategemeana na kazi kubwa Maendeleo ya Wafanyakazi na Wakati ni Sasa"

Mhe. Dkt. Samia alisema kuwa kauli mbiu hiyo inalenga kuhimiza uboreshaji wa maisha ya wafanyakazi kwa upana wake huku akiwataka wafanyakazi kote nchini kuendelea kupatikana ajira zenye usalama na staha kwa watumishi wote nchini.

Akielezea nyongeza za mishahara, Mhe. Rais Dkt. Samia alieleza kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 Serikali itarejesha nyongeza



*Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi.Sarah Mwaipopo (aliyeshika bendera) akifuatilia hotuba ya Mgeni Rasmi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (hayupo pichani) wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Sherehe za Mei Mosi Kitaifa zilizofanyika mkoani Morogoro. Kushoto kwake ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Katiba na Sheria, Bi. Mary Makondo.*

inayofanywa na wafanyakazi wa Serikali na taasisi binafsi ndani ya taifa hili.

Kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi kitaifa ilifanyika katika Viwanja vya Jamhuri Mkoani Morogoro ikiwa na kauli mbiu isemayo, "Mishahara Bora na Ajira za Staha ni Nguzo kwa kufanya kazi kwa uadilifu na weledi kazini kwa kuwa ndio chimbuko la maisha bora kwa wafanyakazi.

Pia, aliwathibitishia wafanyakazi nchini kote kuwa Serikali itaendelea kuboresha maslahi na mazingira ya kazi serikalini na katika sekta binafsi ili za mishahara za mwaka ambazo kwa muda mrefu zilisitishwa. "Nimeona kwa mwaka huu tuzirudishe nyongeza za mishahara kwa wafanyakazi wote, kuna nyongeza za mishahara tunaandaa na tutaendelea kama tulivyokuwa tunafanya zamani", alisema Mhe. Rais Dkt. Samia.

Mbali na upandishaji wa posho, aliongeza kuwa Serikali yake imejiandaa kupandisha madaraja, vyeo vya kimuundo ikiwemo kutenganisha makundi na madaraja mserereko kwa wale ambao hawakupata mwaka jana watapata mwaka huu.

Aidha, alisisitiza kuwa mwaka jana Serikali ilipandisha mishahara kwa asilimia 23.3 ambayo sio kila mtumishi alifaidika kwa sababu lengo hasa lilikuwa ni kuwainua watumishi wa kima cha chini na wengine wachache ingawaje bado kuna kundi kubwa la watumishi halikuguswa.

Naya Naibu Wakili Mkuu wa Serikali, Bi. Sarah Mwaipopo akizungumza mara baada ya Kilele cha Maadhimisho hayo, aliishukuru Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi thabiti wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kuzifanyia kazi changamoto za watumishi ikiwemo nyongeza za mishahara na kupandisha madaraja ya watumishi wote nchini kwa kuwa itawaongezea ari ya utekelezaji wa majukumu yao ipasavyo.




*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakipita mbele ya Mgeni Rasmi, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Mhe. Amos Makala (hayupo pichani) wakati wa Maadhimisho ya Kilele cha Sherehe za Mei Mosi za mkoa huo zilizofanyika uwanja wa Uhuru Jijini Dar es Salaam.*




*Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, James Kibamba (kwanza kulia) akiwa kwenye kiwanja cha Jamhuri Mkoani Morogoro akishiriki kilele cha Maadhimisho ya Sherehe za Mei Mosi Kitaifa.*




*Baadhi ya watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali wakishiriki Kilele cha Maadhimisho ya Sherehe za Mei Mosi Kitaifa Mkoani Mororgoro.*



# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## KURUGENZI YA MAWASILIANO YA RAIS IKULU


*Simu: 255-262961500/1*
*Nukushi: 255-262961502*
*Baruapepe : press@ikulu.go.tz*
*Tovuti : www.ikulu.go.tz*

*OFISI YA RAIS,*
*IKULU,*
*1 BARABARA YA JULIUS NYERERE,*
*CHAMWINO,*
*S.L.P 1102,*
*40400 DODOMA.*


*Dar es Salaam*
*11 Juni, 2023*

## TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan amefanya uteuzi wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) kama ifuatavyo:

i) Amemteua Bw. Frank Kanyusi Frank kuwa Kabidhi Wasii Mkuu. Kabla ya uteuzi Bw. Frank alikuwa Mwanasheria Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mtwara.

Bw. Frank anachukua nafasi ya Bi. Angela Kemanzi Anatory ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

ii) Amemteua Bi. Irene Joseph Lesulie kuwa Naibu Kabidhi Wasii Mkuu. Kabla ya uteuzi Bi. Lesulie alikuwa Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Mashauri ya Kimataifa, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Bi. Irene anachukua nafasi ya Bi. Lina Robert Sanga ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Uteuzi huu umeanza tarehe 08 Juni, 2023.

Zuhura Yunus
Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu

# Mhe. Rais Dkt. Samia amteua Bi. Irene Joseph Lesulie kuwa Naibu Kabidhi Wasii Mkuu - RITA

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, aliwateua viongozi wapya wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) ili kutekeleza majukumu ya taasisi hiyo.

Pamoja na viongozi walioteuliwa kuiongoza taasisi hiyo yenye dhamana ya usajili, ufilisi na udhamini nchini, Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alimteua Bi. Irene Joseph Lesulie kuwa Naibu Kabidhi Wasii Mkuu wa Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA).

Kabla ya utezi huo, Bi. Irene Joseph Lesulie alikuwa Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Mashauri ya Madai ya Kimataifa, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali. Uteuzi huu ulianza tarehe 08 Juni, 2023.

Bi. Irene Lesulie alianza safari ya kitaaluma katika Chuo Kikuu cha Mzumbe huko Morogoro, ambapo alitunukiwa Shahada ya Sheria (LL.B) mwaka 2006. Akiwa katika masomo yake hapo Chuo Kikuu cha Mzumbe, alionyesha uwezo wa kipekee katika kujifunza na kuelewa mambo yote muhimu kwenye taaluma ya Sheria. Jitihada zake katika masomo zilionekana kupitia utendaji wake mzuri wa kitaaluma na ushiriki wake wa dhati katika shughuli mbalimbali za ziada zinazohusiana na nyanja ya sheria.

Mwaka 2015 hadi 2016 Bi. Irene aliendelea na ndoto yake ya kitaaluma kwa kuweza kujiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, ambapo alisomea Shahada ya Uzamili ya Sanaa katika Sheria na Utawala wa Mapato (MARLA). Kupitia masomo hayo, Bi. Lesulie aliweza kupata weledi kwenye sheria za kodi na mapato.

Bi. Irene alijiunga na utumishi wa umma mnamo mwaka 2008 ambapo alianza kazi kama Wakili wa Serikali katika Kurugenzi ya Mashtaka hadi mwaka 2009. Mwaka 2015 hadi 2018 alitumika kwa nafasi ya Wakili wa Serikali na Wakili wa Serikali Mwandamizi, katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali hadi mwaka 2018 ambapo alihamishiwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali ambapo alitumika hadi mwaka 2020 ambapo alipandishwa cheo kuwa Wakili wa Serikali Mkuu na kuteuliwa kwa nafasi ya Kaimu Mkurugenzi Msaidizi wa Katiba, Haki za Binadamu na Uchaguzi.



Mwaka 2021, Bi. Irene Lesulie aliteuliwa kushika nafasi ya Mkurugenzi Msaidizi wa Madai ya Kimataifa na ametumikia wadhifa huo hadi mwaka 2023 alipoteuliwa na Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa wadhifa wa Naibu Kabidhi Mkuu wa Serikali.

Katika safari yake ya kitaaluma, Bi. Lesulie ameonyesha utayari katika kujiendeleza na kushiriki majukumu mbalimbali ya Kitaifa na kimataifa. Mafanikio yake katika utumishi ni ushuhuda wa jitihada zake za kujifunza na kujtoa ili kulitumikia Taifa.




*Naibu Katibu Mkuu- ICSID, Bi. Martina Polasek akiwa katika picha ya pamoja na Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende.*

# *Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali yalenga Kuboresha Mahusiano na Baraza la kimataifa la usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji (ICSID)*

Tarehe 4 Februari, 2023, Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende alipata mwaliko wa kukutana na Katibu Mkuu wa Baraza la kimataifa la usuluhishi wa Migogoro ya Uwekezaji (ICSID), katika Ofisi za ICSID zilizopo jengo la Benki ya Dunia, Washington DC, Marekani, ili kujadili mambo mbalimbali yanayohusu Serikali ya Tanzania na ICSID.

Kutokana na mwaliko huo, tarehe 9 Februari, 2023 Wakili Mkuu wa Serikali, Dkt. Boniphace Luhende akiambatana na watumishi kutoka Ofisi mbalimbali za Serikali ikiwemo, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Rais na Ubalozi wa Tanzania nchini Marekani walihudhuria kikao hicho. Upande wa ICSID uliwakilishwa na Bi Martina Polasek, Naibu Katibu Mkuu wa ICSID, pamoja na Mawakili Bw. Paul Jean Le Cannu na Bi. Ella nberg.

Kupitia kikao hicho, Serikali ilijadiliana mambo mbalimbali ikiwemo mashauri ya Tanzania yaliyofunguliwa katika Baraza la ICSID, mabadiliko ya kanuni za uendeshaji wa mashauri ya Usuluhishi ya ICSID, 2022 yaliyolenga kuongeza uwazi kwenye kuendesha mashauri, kupunguza muda wa kuendesha mashauri na kuongeza ufikiwaji wa Baraza (ICSID). Pia Baraza lilieleza matakwa ya Tanzania kuteua wasuluhishi wanne (4) na wapatanishi wanne (4) katika Baraza la ICSID.

Dkt. Luhende alieleza kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali inaendesha





*Wajumbe katika kikao cha pamoja na Baraza la ICSID, kutoka kushoto ni Paul Jean Le Cannu (Wakili ICSID), Said Nyenge (Afisa Ubalozi) Ipyana Mlilo (Wakili wa Serikali), Bi. Salome Magesa (Mkurugenzi Msaidizi usuluhishi wa kimataifa), Bi. Ella nberg (Wakili ICSID), Bi Martina Polasek, Naibu Katibu Mkuu- ICSID, Dkt. Boniphace Luhende, Wakili Mkuu wa Serikali, George Mandepo (Mkurugenzi Idara ya usuluhishi), Neisha Shao Wakili wa Serikali, Maria Mwakibete (Wakili wa Serikali) na Malik Hassan (Afisa wa ubalozi).*

mashauri ya usuluhishi na madai na ilianzishwa mwaka 2018. Pia, alieleza jitihada mbalimbali zinazofanyika na Ofisi katika kuendesha mashauri hayo ikiwemo kutatua migogoro hiyo kwa majadiliano. Kwa upande wa uendeshaji wa mashauri kwenye Baraza la ICSID ilielezwa kuwa Tanzania imeendesha mashauri mbalimbali ya usuluhishi wa kimataifa kupitia Baraza la ICSID. Pamoja na ushirikiano unaopata kutoka kwenye baraza, bado nchi inakutana na changamoto mbalimbali ikiwemo kitendo cha wawekezaji kubadilisha uraia na kuchukua uraia wa nchi zenye mikataba ya uwekezaji na Tanzania pale kunapozuka migogoro baina yao na Tanzania (Treaty shopping); ukubwa wa tafsiri ya neno wawekezaji na uwekezaji hivyo inafanya nchi iingie gharama kubwa kwa wawekezaji ambao hawakuwekeza; Mabaraza ya ICSID yamekuwa yanatoa gharama/fidia kubwa na za kufikirika kwa wawekezaji bila kujali kiasi halisi cha uwekezaji. Pia, Dkt. Luhende alisitiza na kuomba Baraza lisaidie kutoa mafunzo kwa Mawakili wa Serikali kuhusu uendeshaji wa mashauri ya usuluhishi wa kimataifa.

Baada ya majadiliano hayo ya kina, Baraza la ICSID lilijadili kuwa litaangalia namna bora ya kutoa nafasi kwa Mawakili kupata mafunzo mbalimbali, ikiwemo mafunzo ya nadharia (internship). Pia ilisisitizwa kuwa Serikali ya Tanzania inaweza kupata nafasi ya kujadili matatizo ya kiuwekezaji katika mikutano ya kimataifa ya kikanda ili kuepusha migogoro inayotokana na wawekezaji wasio waadilifu. Endapo kuna maoni yoyote kuhusu utendaji kazi wa Baraza au uendeshaji wa mashauri, Serikali inaweza kuwasilisha maoni yake kwa Katibu Mkuu.

Kwa upande mwingine, Dkt. Luhende alishukuru kwa kikao hicho, na kueleza kuwa itafikisha kwa Serikali umuhimu wa kuteuwa wasuluhishi na wapatanishi katika Baraza la ICSID ili kutoa nafasi kwa watanzania katika kuendesha mashauri ya kimataifa. Vilevile, Tanzania ilialika Baraza la ICSID kuja kufungua Kituo cha Usuluhishi Tanzania ikiwa ni dhamira ya kuunga mkono jitihada za Rais wa Jamhuri ya muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ya kukuza uwekezaji nchini.




**Kuwa wa kwanza kutupata habari na matukio kupitia tovuti ya Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali**

**www.osg.go.tz**

# MAKALA




## Stanley Kalokola

Wakili wa Serikali


# *Jaji mmoja ana mamlaka ya kusikiliza shauri la kikatiba lisilohusu haki za Binadamu*

*Na Stanley Kalokola*

Uendeshaji wa mashauri yanayohusu Katiba umepata mtazamo mpya baada ya Mahakama Kuu ya Tanzania kuamua kwamba Jaji mmoja ana mamlaka ya kusikiliza shauri la kikatiba. Mtazamo huu wa kisheria umetokana na mapingamizi ya kisheria ambayo upande wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali imekuwa ikiweka pingamizi kuhusu mamlaka ya Jaji mmoja kusikiliza shauri la kikatiba. Mapingamizi haya yamekuwa yakiwekwa katika mashauri ambayo yamekuwa yakipangwa mbele ya Jaji mmoja. Msingi wa mapingamizi umekuwa ukizingatia uzoefu kwamba mashauri ya kikatiba yanasikilizwa na jopo la Majaji watatu baada ya kutungwa Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu, Sura ya 3 ya Sheria za Tanzania "The Basic Rights and Duties Enforcement Act, [Cap 3. R.E 2019].

Kabla ya mwaka 1994, mashauri ya kikatiba yawe ya haki za binadamu au hoja nyingine yalikuwa yakisikilizwa na Jaji mmoja. Hii ni kwa sababu ibara ya 30(3) inayoruhusu mashauri kuhusu uvunjaji wa haki za binadamu zinazotambulika katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 hayakuwa yametungiwa sheria ya kutoa mwongozo wa namna Mahakama Kuu ya Tanzania inavyoweza kuyasikiliza. Mamlaka ya kutunga sheria yakusimamia mashauri ya haki za binadamu

yanatamkwa na ibara ya 30(4) ya Katiba ya Tanzania. Kwa upande mwingine, mambo yote ambayo katiba au sheria haijatoa utaratibu wa mahakama ipi iyasikilize, ibara ya 108(2) ya Katiba ya Tanzania inaipa mamlaka Mahakama Kuu kuweza kusikiliza mambo hayo kwa kuzingatia utaratibu na desturi za Mahakama Kuu. Hivyo, kwa mujibu wa Katiba, Mahakama Kuu inaweza kusikiliza mashauri ya haki za binadamu kwa utaratibu uliyowekwa na Sheria kwa mujibu wa Ibara ya 30(3) na 30(4) na kusikiliza jambo lingine kwa mamlaka yaliyopo katika Ibara ya 108(2) ya Katiba ya Tanzania.

Itakumbukwa kwamba kabla ya kutungwa kwa Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu "The Basic Rights and Duties Enforcement Act" mwaka 1995, mashauri ya haki za binadamu yalikuwa yakisikilizwa na Jaji mmoja. Mathalani shauri kati ya Mchungaji Christopher Mtikila dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Shauri la Madai Na.5 la Mwaka 1993, Mahakama Kuu - Dodoma. Shauri hili lilikuwa linapigania haki ya kuwa na mgombea binafsi katika uchaguzi lilisikilizwa na Jaji mmoja, Jaji K.S.K Lugakingira au Shauri la Maombi ya Dhamana Na. 80 ya Mwaka 1988 kati ya Daudi Pete dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka yaliyoamua kwamba kifungu cha 148(5) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kinachozuia utoaji wa dhamana kwa baadhi ya makosa kuwa ni kinyume na Katiba na kwamba kinavunja haki za binadamu hususani haki ya kupata dhamana. Shauri hili pia liliamuliwa na Jaji mmoja, Mhe. Jaji Mwalusanya.

Msimamo wa Mahakama ya Rufaa kuhusu utaratibu wa kusikiliza mashauri ya haki za binadamu chini ya Ibara ya 30(3) na 30(4) ya Katiba ya Tanzania ilikuwa ni kwamba Mahakama Kuu itawajibika kutumia taratibu na mazoea yanayotumika katika Mahakama Kuu mpaka pale Bunge litakapotunga sheria ya kuweka utaratibu wa kuendesha mashauri hayo. Uamuzi huu ulitolewa katika Shauri la Rufaa ya Jinai Na. 28 ya mwaka 1990 kati ya Mkurugenzi wa Mashtaka dhidi ya Daudi Pete mbele ya jopo la Majaji watatu wa Rufaa likiongozwa na Jaji Mkuu Nyalali, Jaji Makame na Jaji Ramadhani. Baada ya kutungwa Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu mwaka 1995, mashauri ya kikatiba yanayohusu haki za binadamu yalitakiwa kusikilizwa na Mahakama Kuu chini ya jopo la majaji watatu. Hii ni kwa mujibu wa kifungu cha 10(1) cha Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu. Hivyo, utaratibu wa Jaji mmoja kusikiliza shauri la kikatiba kuhusu haki za binadamu ulibadilika jambo ambalo liliathiri hata mashauri ya kikatiba ambayo hayakuhusu haki za binadamu nayo yalianza kusikilizwa na majaji watatu kupitia Ibara ya 26(2) ya Katiba ambayo inatoa wigo mkubwa kwa mtu yeyote kuchukua hatua ya kwenda mahakamani kwa lengo la kulinda Katiba au sheria yoyote isivunjwe.

Mwaka 2020, Bunge lilifanya marekebisho katika Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali "The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Act, No. 3 of 2020". Sheria hii ilifanya marekebisho yaliyotaka Ibara ya 26(2) isomwe sambamba na Ibara ya 30(3) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hii ni pamoja na kuongeza takwa la kisheria kwa mtu anayelalamika kuvunjwa kwa Katiba au sheria yoyote kwa kupitia Ibara ya 26(2) na 30(3) kuapa kiapo kinachoonesha namna ambavyo yeye binafsi ameathirika na jambo analolilalamikia. Kwa mtazamo wa wengi marekebisho hayo yalionekana kutaka kuminya haki ya kuleta mashauri ya kikatiba kwa maslahi mapana ya umma kwa uwepo wa takwa la kiapo kinachoonesha namna mlalamikaji alivyoathirika binafsi na jambo analolilalamikia. Hii ilisababisha kufunguliwa kwa Shauri la kikatiba lililokuwa linapinga marekebisho

hayo ya Sheria. Shauri hilo ni Shauri la kikatiba Na. 9 la Mwaka 2021 kati ya Onesmo Olengurumwa dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Shauri hili lilisikilizwa na jopo la Majaji watatu ambao ni Jaji Mlyambina, Luvanda na Magoiga. Katika Shauri hili, Mahakama ilikubaliana na hoja za Serikali kuwa marekebisho hayo ya sheria hayaminyi uhuru wa kuleta shauri la kikatiba kwa maslahi mapana ya umma ila sheria imeweka chujio ili kuruhusu tu mashauri yenye tija kuja Mahakamani na sio yale yenye lengo la kutafuta umaarufu wa kisiasa au namna nyingine yoyote au yasiyokuwa na mantiki.

Kutokana na uamuzi huo, wanaharakati walianza kutafuta mbinu mbadala ya kuleta mashauri ya kikatiba pasipo kukutana na masharti ya kuonesha namna wanavyoathirika na jambo husika kupitia Ibara ya 26(2) na 30(3) ya Katiba. Katika mchakato huo, ndipo wanaharakati walianza kutumia Ibara ya 108(2) ya Katiba kuleta mashauri ya kikatiba hususani yale yasiyohusu haki za binadamu. Hoja ikawa je ni utaratibu gani utatumika kuyaongoza mashauri yanayofunguliwa chini ya Ibara ya 108(2) ya Katiba? Je Mahakama Kuu inatakiwa kuwa na jopo la majaji wangapi katika kusikiliza mashauri hayo? Mashauri yaliyofunguliwa chini ya Ibara ya 108(2) ya Katiba tangu mwaka 2020 ni pamoja na Odero Charles Odero dhidi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na wenzake wawili, Shauri Na. 21 la Mwaka 2021(shauri lilihoji mamlaka ya Mkurugenzi wa Mashtaka kufungua shauri la jinai kabla ya upelelezi kukamilika), James Francis Mbatia dhidi ya Job Yustino Ndugai na wenzake wawili, Shauri Na. 2 la Mwaka 2022 (shauri hili lilihoji kutofuatwa kwa utaratibu wa kikatiba wa kujiuzuru kwa Spika wa Bunge), Tito Elias Magoti dhidi ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi na wenzake watatu, Shauri Na. 3 la Mwaka 2022 (Shauri hili lilikuwa linahoji haki za wafungwa kupiga kura katika uchaguzi mkuu) pamoja na Paul Kilasa Kisabo dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Shauri Na. 9 la Mwaka 2022 (Mamlaka ya Rais kuweza kumvua wadhifa Jaji Mkuu).

Katika Shauri la Odero Charles Odero, Mahakama iliamua kwamba shauri linalofunguliwa chini ya Ibara ya 108(2) ya Katiba, mlalamikaji habanwi na masharti yaliyomo katika Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu. Katika shauri hili licha ya kuletwa chini ya Ibara ya 108(2) ya Katiba lilisikilizwa na jopo la majaji watatu ambao ni Jaji Mgeta, Masoud na Kakolaki. Uamuzi huu ukafuatwa kwenye shauri la James Francis Mbatia dhidi ya Job Yustino Ndugai. Katika Shauri la Tito Elias Magoti dhidi ya Tume ya Uchaguzi ambalo nalo lililetwa chini ya Ibara ya 108(2) ya Katiba, hoja ilikuwa kama Jaji mmoja anaweza kusikiliza shauri la kikatiba. Katika kujibu hoja hii, Mahakama iliamua kuwa shauri la kikatiba linaloletwa chini ya Ibara ya 108(2) ya Katiba kama halihusu haki za binadamu linaweza kusikilizwa na Jaji mmoja, uamuzi uliotolewa na Jaji Luvanda. Uamuzi huu wa Jaji mmoja kuwa na uwezo wa kusikiliza shauri la kikatiba lisilohusu haki za binadamu ukafuatwa kwenye shauri la Paul Kilasa Kisabo dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Hivyo, kwa sasa msimamo wa kisheria katika Mahakama Kuu ya Tanzania ni kwamba Jaji mmoja anayo mamlaka ya kisheria kuweza kusikiliza shauri la kikatiba ambalo halihusu haki za binadamu. Hii ni kwa sababu mashauri ya haki za binadamu zinazotambulika katika Ibara ya 12-29 ya Katiba yamewekewa utaratibu wake kupitia Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu, Sura ya 3 ya Sheria za Tanzania. Msimamo huu unazingatia kwamba Ibara ya 108(2) ya Katiba haijatungiwa sheria ya kuongoza mashauri yanayoletwa chini yake. Hivyo, kwa sasa Mahakama Kuu imekuwa ikitumia taratibu na desturi za Mahakama Kuu katika kuendesha mashauri haya

ya kikatiba. Taratibu hizo zinaweza kukopwa katika Sheria mbalimbali za uendeshaji wa mashauri ya madai kama vile Sheria ya Mwenendo wa mashauri ya Madai "The Civil Procedure Code", Sheria ya Ushahidi "The Evidence Act" na Sheria nyingine kulingana na mazingira ya jambo husika. Hivyo kwa sasa, shauri la kikatiba chini ya Ibara ya 108(2) ya Katiba linaweza kupangwa mbele ya Jaji mmoja au Jopo la Majaji watatu kwa namna ambavyo Jaji Kiongozi ataona inafaa.

Ni mtazamo wangu kwamba msimamo wa Mahakama Kuu kuruhusu Jaji mmoja kusikiliza shauri la kikatiba unaweza kuwa na changamoto kidogo kulingana na ukweli kwamba mashauri ya uvunjwaji wa katiba ni mashauri nyeti sana. Hii inatokana na ukweli kwamba Katiba ni chimbuko la Sheria na mamlaka yote ndani ya nchi, hivyo jambo la kikatiba ni jambo nyeti sana. Hivyo, uwepo wa Jopo la Majaji watatu linaongeza uzito na uwepo wa Mahakama kutumia uwezo kufafanua kwa kina hoja kwa kutumia majaji watatu. Hii itasaidia kutofautisha uzito wa mashauri ya kikatiba na mashaurimengineyakawaida katika Mahakama Kuu ambayo husikilizwa na Jaji mmoja. Hii ndiyo mana Jaji Lugakingira kwenye Shauri la Mchungaji Christopher Mtikila dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali [1995] TLR 31 alisema uvunjwaji wa katiba ni suala nyeti na baya sana ambalo haliwezi kuamuliwa kwa maelezo ya juu juu isipokuwa uthibitisho usiokuwa na mashaka "*Breach of the Constitution is such a grave and serious matter that cannot be established by mere inference but by proof beyond reasonable doubt*". Hivyo, kwa mtazamo wangu kwa mashauri yanayoletwa chini ya Ibara ya 108(2) ya Katiba yana uzito sawa na mashauri ya haki za binadamu. Hivyo Mahamakama ingeweza kuchukua uzoefu na desturi iliyopo sasa ya Jopo la Majaji watatu kusikiliza shauri la kikatiba kuhusu haki za binadamu kama ilivyo kwenye Sheria ya Utekelezaji wa Haki na Wajibu.

Msingi mwingine wa mtazamo wa kuwa na jopo la majaji watatu unatokana na kwamba mfumo wa Katiba ya Tanzania unatoa uzito sawa kwa ibara zote. Hivyo hakuna sehemu katika Katiba ambayo ina uzito zaidi ya sehemu nyingine. Msimamo huu unatokana na kwamba hata utaratibu wa kufanya mabadiliko ya kwenye katiba kwa mujibu wa Ibara ya 98 ya Katiba yanaruhusu sehemu yoyote ya katiba kubadilishwa na hivyo kufanya sehemu zote za katiba kuwa na uzito sawa. Mtazamo huu unaungwa mkono na mtazamo wa Majaji Saba wa Mahakama ya Rufaa katika Shauri la Rufaa Na. 45 la Mwaka 2009 kati ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali dhidi ya Mchungaji Christopher Mtikila. Katika Shauri hili, Mahakama ya Rufani iliamua kwamba Katiba ya Tanzania haina sehemu ambayo haiwezi kubadilishwa kwa mamlaka ya Bunge kupitia utaratibu wa Ibara ya 98 ya Katiba ya Tanzania. Hii ni kwa sababu sehemu zote ziko sawa na hakuna kitu kinaitwa "Basic Structure" kwenye Katiba ya Tanzania.

Mwisho, kwa kuwa hakuna sheria inayosimamia mashauri yanayofunguliwa chini ya Ibara ya 108(2) ya Katiba, nashauri Bunge kwa mamlaka yake itunge sheria ya kuiongoza Mahakama Kuu inaposikiliza mashauri ya kikatiba yasiyohusu haki za binadamu kupitia Ibara ya 108(2) ya Katiba ya Tanzania. Hii itasaidia kuwa na utaratibu unaoeleweka na kufanya maamuzi ya Mahakama kutabirika kuliko sasa ambapo hakuna utaratibu isipokuwa busara ya Mahakama kwa kupitia uzoefu na desturi ya Mahakama Kuu. Kutabirika katika Mahakama ni muhimu sana kwa sababu kila jambo linakuwa wazi kwenye sheria kuanzia masuala ya kuwekwa kwenye nyaraka, mamlaka ya Mahakama, mfumo wa Ushahidi na mengineyo.

# TANZIA



## DKT. ABDUL MUSSA ALLY
### MKURUGENZI WA MIPANGO
### OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

**1971 - 2023**



*Nainu Wakili Mkuu wa Serikali Sarah Mwaipopo akitoa Salaam za Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kwa waombolezaji waliofika kumsindikiza katika safari yake ya mwisho aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Mipango Dkt. Abdul Mussa Ally Jijini Dar es Salaam.*

# Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo aliwaongoza watumishi wa OWMS kumuaga Dkt. Abdul Mussa Ally

Naibu Wakili Mkuu wa Serikali Bi. Sarah Mwaipopo aliwaongoza watumishi wa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali kumuaga aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Mipango Dkt. Abdul Mussa Ally aliyefariki kwa ajali ya gari iliyotokea Mdaula mkoani Pwani siku ya jumapili tarehe 23 April 2023.

Akizungumzia namna walivyoguswa na msiba huo Bi. Mwaipopo alisema kuwa Ofisi ya Wakili Mkuu Serikali na watumishi wote tumepokea taarifa hizi kwa simanzi kubwa kwa sababu tumempoteza mtu muhimu kwa familia, Ofisi na Taifa kwa ujumla. "Ajali hii imegharimu maisha yake na ameondoka kwetu ghafla na mapema mno angali bado tunamhitaji", alisema Bi. Mwaipopo.

Aliongeza kuwa Dkt. Abdul Mussa Ally alikuwa mtumishi mahiri, hodari, mchapakazi, na mbobevu katika masuala ya Uchumi, Mipango na Usimamizi wa Fedha. Katika kipindi chote cha utumishi

wake, marehemu alijitoa kikamilifu katika ujenzi wa Taifa na daima alitumia ujuzi na maarifa yake yote katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Akizungumzia masuala mbalimbali yaliyotekelezwa na Dkt. Abdul Mussa Ally, kiongozi huyo alisema kuwa akiwa mchumi mbobevu, alihakikisha kuwa Ofisi inapata ongezeko la bajeti ya Matumizi Mengineyo kutoka Shilingi Bilioni Tisa (9,028,155,000/=) mwaka 2021/2022 hadi kufikia shilingi bilioni kumi na tatu nukta nne(13,446,669,000/=) mwaka 2023/24 ambapo kulikuwa na ongezeko la shilingi bilioni nne nukta nne (4,418,514,000/=).

Akielezea majukumu mengine yaliyotekelezwa na Dkt. Abdul Mussa Ally enzi za uhai wake, Naibu Wakili Mkuu wa Serikali alisema kuwa Marehemu Dkt. Mussa alisimamia Mapitio ya Mpango Mkakati wa Miaka Mitano ambao umeanza mwaka 2021/2022 hadi mwaka 2025/2026.

Aidha, Dkt. Abdul Mussa Ally alisimamia maandalizi ya Mpango Kazi wa Ofisi (Action Plan) kuanzia mwaka 2020/2021 hadi Mwaka huu wa Fedha 2022/2023, ikiwa ni pamoja na kushiriki kwenye mijadala mbalimbali inayohusu masuala ya Mipango na Bajeti iliyoandaliwa na Wizara ya Fedha na Mipango ambapo mijadala hiyo ilileta tija kwenye masuala mbalimbali ya kibajeti kwa Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali.

Alifafanua kuwa Dkt. Abdul Mussa Ally alikuwa kiongozi mahiri katika kusimamia uandaaji wa mipango ya kila mwaka, matayarisho ya bajeti, ufuatiliaji wa utekelezaji wa bajeti, uandaaji wa taarifa za bajeti pamoja na taarifa za kila mwaka za Ofisi.

Kiongozi huyo aliwashukuru waombolezaji wote, huku akiwataka waombolezaji hao kuwa tumuenzi marehemu kwa kudumisha kumbukumbu zake nzuri na kuendeleza mema yote aliyotuachia.

Naye Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Uchukuzi, Dkt. Ally Possi alimuelezea Dkt. Abdul Mussa Ally kama mtu mwenye maarifa na weledi mkubwa hivyo Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali na Taifa kwa ujumla imempoteza mtu shujaa na Mchapakazi.

Aliongeza kuwa Dkt. Abdul Mussa Ally alikuwa kiongozi shupavu aliyekuwa tayari kutekeleza majukumu kwa ufanisi mkubwa pamoja na kutoa msaada wowote pale inapohitajika kwa ajili ya kuhakikisha analiletea taifa letu maendeleo.

Dkt. Abdul Mussa Ally alizaliwa tarehe 05 Februari, 1971 huko Ujiji mkoani Kigoma, ameacha Mke na Watoto.



*Baadhi ya waombolezaji waliofika kumsindikiza katika safari yake ya mwisho aliyekuwa Mkurugenzi wa Idara ya Mipango Dkt. Abdul Mussa Ally Jijini Dar es Salaam.*

JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA

# OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI

**OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI**
**10 Barabara ya Kivukoni**
**S. L. P 71554**
**11101 DAR ES SALAAM**

**Simu: +255 22 2127384**
**Fax: +255 22 2127385**
**Nukushi: www.osg.go.tz**
**Barua pepe: info@osg.go.tz**

## ANUANI ZA POSTA NA MAENEO ZILIPO OFISI ZA WAKILI MKUU WA SERIKALI MIKOANI

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 1902
41218 DODOMA
Jengo la Katiba na Sheria (UDOM)
Barua pepe: dodoma@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 130
31101 MUSOMA
Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Barua pepe: mara@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 1280
63114 MTWARA
Maadili House
Barua pepe: mtwara@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 394
33101 MWANZA
Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Barua pepe: mwanza@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 595
51108 IRINGA
Lilokuwa jengo la Halmashauri ya Wilaya ya Iringa
Barua pepe: iringa@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 106
35102 BUKOBA
Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Mhakiki Mali
Barua pepe: kagera@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 564
57101 SONGEA
Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Barua pepe: ruvuma@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 43
37101 SHINYANGA
Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Barua pepe: shinyanga@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 60
21101 TANGA
Jengo la Mkonge
Barua pepe: tanga@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 119
45112 TABORA
Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Mkoa
Barua pepe: tabora@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 202
25101 MOSHI
Jengo la TRA Moshi
Barua pepe: kilimanjaro@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 690
55103 SUMBAWANGA, Mtaa wa Ukaguzi
Jengo la Ukaguzi, Gorofa ya pili
Barua pepe: rukwa@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 66
23101 ARUSHA
Jengo la AICC, Arusha
Barua pepe: arusha@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 710
53107 MBEYA
Jengo la Madini
Barua pepe: mbeya@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
S. L. P 172
47101 KIGOMA, Jengo la NHC, Ghorofa ya Pili,
Kiwanja Na. 148 & 149, Mtaa wa Lumumba.
Barua pepe: kigoma@osg.go.tz

OFISI YA WAKILI MKUU WA SERIKALI
Jengo la NSSF, Ghorofa la Nne
MOROGORO, Barabara ya zamani DSM
Barua pepe: morogoro@osg.go.tz